

TANGAZO

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania anapenda kuwajulisha watu wote wanaotaka kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne (**CSEE**) na Maarifa (**QT**) mwezi **Novemba, 2017** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha usajili cha watahiniwa kitaanza tarehe **1 Januari, 2017** kwa ada ya Shilingi **50,000/=** kwa wanaojisajili **CSEE** na Shilingi **30,000/=** kwa wanaojisajili **QT** na kitaishia tarehe **28 Februari, 2017**. Aidha, watakojisajili kwa kuchelewa kuanzia tarehe **01/03/2017** hadi tarehe **31/03/2017** watalipa Shilingi **65,000/=** kwa watahiniwa wa Kidato cha Nne (**CSEE**) na Shilingi **40,000/=** kwa watahiniwa wa mtihani wa Maarifa (**QT**) ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
2. Mtahiniwa atakaye jisajili kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne (**CSEE**) **2017** ni yule ambaye anarudia Mtihani wa Kidato cha Nne (**CSEE**) au amefanya na kufaulu Mtihani wa Maarifa (**QT**) katika kipindi kisichozidi miaka mitano (**5**) iliyopita **au** mwenye sifa zinazolingana na hizo alizopata kutoka nje ya Nchi na kufanyiwa ulinganifu na Baraza la Mitihani la Tanzania.
3. Mtahiniwa atakaejisajili kufanya Mtihani wa Maarifa ni yule ambaye anatafuta sifa ya kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne kama Mtahiniwa wa kujitegemea.
4. Kabla ya kujisajili kwenye mtandao, waombaji wanapaswa kwenda kwenye vituo vya mitihani kuchukua namba rejea (**reference number**) zinazotolewa **bure** na kufanya malipo ya ada ya mtihani katika ofisi za **Posta pekee**.
5. Waombaji wote **wanasisitizwa** kuhakikisha wanajisajili mapema kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Baraza la Mitihani ya www.necta.go.tz kwani mfumo wa usajili utafungwa baada ya kipindi cha usajili kumalizika.

Imetolewa na:

KATIBU MTENDAJI